**CHAMA CHA WAFANYAKAZI WA SERIKALI ZA MITAA TANZANIA (TALGWU)**

# TANGAZO LA UCHAGUZI WA TALGWU KWA NGAZI YA MATAWI, WILAYA, MIKOA NA TAIFA 2026

Chama cha Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa Tanzania (TALGWU) kinawatangazia Wanachama wote kwamba kutakuwa na uchaguzi mkuu wa ngazi ya Matawi, Wilaya Mikoa na Taifa utakaofanyika kuanzia mwezi Aprili 2026 na kukamilika mwezi Septemba 2026. katika uchaguzi huo, watachaguliwa viongozi wa kukiongoza Chama kwa kipindi cha miaka mitano. Ratiba ya chaguzi hizo na maeneo ya kuchukua na kurejesha fomu, sifa za wagombea na nafasi za uongozi zitakazogombewa ni kama ifuatavyo:

## 1. UCHAGUZI WA MATAWI

### 1.1 Muda wa kuchukua na kurejesha fomu

i. Tarehe 23 - 27 Machi 2026 ni Kuchukua na kurejesha fomu.

ii. Muda wa kuchukua fomu ni kuanzia saa 2:00 asubuhi hadi saa 9:30 alasiri ya kuanzia tarehe 23 Machi 2026 na mwisho wa kurejesha fomu hizo katika Ofisi za Matawi ni saa 9:30 alasiri tarehe 27 Machi 2026.

iii. Fomu za kugombea uongozi zitatolewa bure katika Matawi yote Tanzania Bara.

iv. Kila Mwanachama anayetaka kugombea atachukua na kurejesha fomu kwa Katibu wa Tawi lake anapofanyia kazi.

v. Uchaguzi wa Matawi utafanyika kuanzia tarehe 22 Aprili hadi tarehe 12 Juni 2026.

## 1.2 Sifa za wagombea uongozi katika Matawi

a) Awe raia wa Tanzania.

b) Awe Mwanachama wa TALGWU kwa kipindi kisichopungua mwaka mmoja na kuendelea.

c) Awe muadilifu na asiwe na historia ya makosa ya jinai.

d) Wagombea wa nafasi ya Vijana; wahakikishe kwamba umri wao wakati wa kugombea uwawezeshe kukitumikia Chama si chini ya miaka mitano (5) baada ya kuchaguliwa kabla ya umri wa ujana wake kuisha.

## 1.3 Nafasi za uongozi zinazogombewa katika Tawi:

i. Wajumbe watano akiwemo Mwenyekiti na Katibu wa Tawi kama Tawi lina wanachama kumi na sio zaidi ya wanachama hamsini.
ii. Wajumbe kumi ambao ni pamoja na Mwenyekiti na Katibu wa Tawi kama Tawi linazidi wanachama hamsini lakini chini ya mia moja.
iii. Wajumbe kumi na tano ambao ni pamoja na Mwenyekiti na Katibu wa Tawi kama Tawi lina wanachama wanaozidi mia moja lakini chini ya mia tano.
iv. Wajumbe ishirini ambao ni pamoja na Mwenyekiti na Katibu wa Tawi kama Tawi lina wanachama wanaozidi mia tano lakini chini ya elfu moja.
v. Mwenyekiti na Katibu wa Kamati ya Ushauri ya Wafanyakazi Wanawake wa Tawi.
vi. Wajumbe wawili wa Kamati ya Ushauri Wafanyakazi Wanawake
vii. Mwakilishi wa Wafanyakazi vijana wa Tawi.
viii. Mwakilishi wa Wafanyakazi wenye ulemavu katika Tawi.

## 2.0 UCHAGUZI WA WILAYA

### 2.1 Muda wa kuchukua na kurejesha fomu

i. Tarehe 23 - 27 Machi 2026 ni kuchukua na kurejesha fomu.
ii. Muda wa kuchukua fomu ni kuanzia saa 2:00 asubuhi hadi saa 9:30 alasiri kuanzia tarehe 23 Machi 2026 na mwisho wa kurejesha fomu hizo katika Ofisi za Matawi ni saa 09:30 alasiri tarehe 27 Machi, 2026.
iii. Fomu za kugombea uongozi zitatolewa bure katika Matawi yote Tanzania Bara.
iv. Kila Mwanachama anayetaka kugombea atachukua na kurejesha fomu kwa Katibu wa Tawi lake anapofanyia kazi.
v. Uchaguzi wa Wilaya utafanyika kuanzia tarehe 22 Juni 2026 hadi tarehe 04 Julai 2026.

### 2.2 Sifa za wagombea uongozi katika Wilaya

a) Awe raia wa Tanzania.

b) Awe Mwanachama wa TALGWU kwa kipindi kisichopungua mwaka mmoja na kuendelea.

c) Awe muadilifu na asiwe na historia ya makosa ya jinai.

d) Wagombea wa nafasi ya Vijana; wahakikishe kwamba umri wao wakati wa kugombea uwawezeshe kukitumikia Chama si chini ya miaka mitano (5) baada ya kuchaguliwa kabla ya umri wa ujana wake kuisha.

### 2.3 Nafasi za uongozi zinazogombewa katika Wilaya:

(a) Mwenyekiti wa Wilaya atakayetoka miongoni mwa Wenyeviti wa Matawi.
(b) Mjumbe mmoja kutoka miongoni mwa Makatibu wa matawi atakayeingia kwenye Kamati ya Utendaji ya Wilaya.
(c) Mjumbe mmoja anayewakilisha Wilaya kwenye Kamati ya Utendaji Mkoa.
(d) Mwenyekiti na Katibu wa Kamati ya Ushauri ya Wafanyakazi

Wanawake wa Wilaya.

(e) Wajumbe watatu wa Kamati ya ushauri Wafanyakazi wanawake

(f) Mjumbe mmoja kutoka miongoni mwa wafanyakazi wanawake anayewakilisha Wilaya kwenye Kamati ya ushauri Wafanyakazi wanawake Mkoa.

(g) Mwakilishi wa Wafanyakazi Vijana atakayewakilisha vijana kwenye Kamati ya Utendaji ya Wilaya kutoka miongoni mwa wawakilishi wa Vijana wa Matawi.

(h) Mwakilishi wa Wafanyakazi wenye ulemavu atakayewakilisha Wafanyakazi wenye ulemavu kwenye Kamati ya Utendaji ya Wilaya kutoka miongoni mwa wawakilishi wa wenye ulemavu wa Matawi.

(i) Wawakilishi watatu (3) watakaoingia kwenye Kamati ya Utendaji ya Wilaya kutoka miongoni mwa Wanachama wanaofanya kazi Serikali Kuu, Wakala na Taasisi za Serikali.

(j) Wajumbe watatu (3) kwa kuzingatia jinsia watakaowakilisha Wilaya kwenye Mkutano Mkuu wa Mkoa.

## 3.0 UCHAGUZI WA MIKOA

### 3.1 Muda wa kuchukua na kurejesha fomu

i. Tarehe 23 - 27 Machi 2026 ni wagombea kuchukua na kurejesha fomu.

ii. Muda wa kuchukua fomu ni kuanzia saa 2:00 asubuhi hadi saa 9:30 alasiri kuanzia tarehe 23 Machi 2026 na mwisho wa kurejesha fomu hizo katika Ofisi za Mkoa ni saa 9:30 alasiri tarehe 27 Machi, 2026.

iii. Fomu za kugombea uongozi zitatolewa bure katika ofisi za Matawi/Mikoa yote Tanzania Bara.

iv. Kila Mwanachama anayetaka kugombea atachukua fomu kwa Katibu wa Tawi/Mkoa na kurejesha fomu hizo yeye mwenyewe kwa Katibu wa Mkoa wake anapofanyia kazi.

v. Uchaguzi wa Mikoa utafanyika kuanzia tarehe 13 Julai 2026 hadi tarehe 04 Septemba 2026.

### 3.2 Sifa za wagombea uongozi katika ngazi ya Mikoa

a) Awe raia wa Tanzania.

b) Awe muadilifu na asiwe na historia ya makosa ya jinai.

c) Kwa nafasi ya Mwenyekiti wa Mkoa, Mjumbe wa Baraza Kuu Taifa na Mjumbe wa Kamati ya Utendaji Taifa wawe Wanachama sio chini ya miaka mitano (5) na wawe walishawahi kushika nafasi ya Ujumbe wa Kamati ya Utendaji Mkoa/Ujumbe wa Kamati ya Ushauri Wafanyakazi Wanawake Mkoa na wamehudumu katika nafasi hiyo kwa kipindi kisichopungua miaka mitano (5).

d) Kwa nafasi ya Mjumbe wa Mkutano Mkuu TUCTA wawe Wanachama sio chini ya miaka mitano (5) na wawe walishawahi kushika nafasi ya Uongozi/Mjumbe wa Kitaifa katika Chama na kuhudumu katika nafasi hiyo kwa kipindi kisichopungua miaka mitano (5).

e) Kwa nafasi ya Mjumbe wa Mkutano Mkuu Taifa wawe wanachama sio chini ya miaka mitano (5) na wawe walishawahi kushika nafasi yeyote ya uongozi

katika Wilaya/Mkoa na wamehudumu katika nafasi hiyo kwa kipindi kisichopungua miaka mitano (5).

f) Wagombea wa nafasi ya Vijana; wahakikishe kwamba umri wao wakati wa kugombea awe ana uwezo wa kukitumikia Chama si chini ya miaka mitano (5) baada ya kuchaguliwa kabla ya umri wa ujana wake kuisha.

**3.3 Nafasi za uongozi zinazogombewa katika Mikoa:**

a) Mwenyekiti wa Mkoa.
b) Mjumbe mmoja wa Baraza Kuu la Taifa atayewakilisha Mkoa.
c) Mjumbe mmoja wa Kamati ya Utendaji Taifa atakayewakilisha Mkoa.
d) Wajumbe watatu (3) watakaowakilisha Mkoa katika Mkutano Mkuu wa Taifa kwa kuzingatia jinsia.
e) Mwenyekiti wa Kamati ya Ushauri Wafanyakazi Wanawake Mkoa.
f) Katibu wa Kamati ya Ushauri Wafanyakazi Wanawake Mkoa.
g) Mwakilishi wa Shirika la Maendeleo la Uchumi lililopo katika Mkoa.
h) Mjumbe mmoja mwakilishi wa watu wenye ulemavu kuwa mjumbe wa Kamati ya Utendaji Mkoa kutoka miongoni mwa wawakilishi wa Wafanyakazi wenye ulemavu wa Wilaya.
i) Mjumbe mmoja mwakilishi wa vijana kuwa mjumbe wa Kamati ya Utendaji Mkoa kutoka miongoni mwa wawakilishi wa vijana wa Wilaya.
j) Wajumbe watatu (3) wanaoingia kwenye Kamati ya Utendaji Mkoa kutoka miongoni mwa Wanachama wanaofanya kazi Serikali Kuu, Wakala na Taasisi za Serikali.
k) Wajumbe watatu (3) wa Mkutano Mkuu wa Mkoa kutoka miongoni mwa Wanachama wanaofanya kazi Serikali Kuu, Wakala na Taasisi za Serikali.
l) Mjumbe mmoja anayewakilisha Chama katika Mkutano Mkuu wa Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania (TUCTA).

## 4.0 UCHAGUZI WA TAIFA

**Muda wa kuchukua na kurejesha fomu**

i. Tarehe 23 - 27 Machi, 2026 ni wagombea kuchukua na kurejesha fomu.

ii. Muda wa kuchukua fomu ni kuanzia saa 2:00 asubuhi hadi saa 9:30 alasiri kuanzia tarehe 23 Machi, 2026 na mwisho wa kurejesha fomu hizo katika Ofisi ya Mkoa ni saa 9:30 alasiri tarehe 27 Machi, 2026.

iii. Fomu za kugombea uongozi zitatolewa bure katika Mikoa yote Tanzania Bara.

iv. Kila Mwanachama anayetaka kugombea atachukua fomu kwa Katibu wa Tawi/ Mkoa na Mwombaji anatakiwa kuwasilisha fomu zake yeye binafsi au kwa kutuma kwa rejista na ahakikishe kuwa fomu yake itafika panapo husika na kwa muda uliowekwa.

v. Mkutano Mkuu wa Uchaguzi wa Taifa utafanyika tarehe 18 Septemba 2026 na Uchaguzi wa Baraza Kuu utafanyika tarehe 19 Septemba 2026.

## 4.1 Sifa za wagombea uongozi katika ngazi ya Taifa

a) Awe raia wa Tanzania.

b) Awe muadilifu na asiwe na historia ya makosa ya jinai.

c) Kwa nafasi ya Mwenyekiti wa Taifa, Makamu Mwenyekiti, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Mweka hazina wa Chama Taifa, Wadhamini wa Chama, Mwenyekiti na Katibu wa Kamati ya Ushauri Wafanyakazi Wanawake Taifa wawe Wanachama sio chini ya miaka mitano (5) na wawe walishawahi kushika nafasi ya Uongozi/Mjumbe wa Kitaifa katika Chama na kuhudumu katika nafasi hiyo kwa kipindi kisichopungua miaka mitano (5).

d) Kwa nafasi ya Mjumbe wa Baraza Kuu TUCTA wawe Wanachama sio chini ya miaka mitano (5) na wawe walishawahi kushika nafasi ya

Uongozi/Mjumbe wa Kitaifa katika Chama na kuhudumu katika nafasi hiyo kwa kipindi kisichopungua miaka mitano (5).

e) Kwa nafasi ya Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu wa Chama ni lazima wawe na elimu ya shahada ya kwanza au zaidi, au sifa zinazolingana na hizo kutoka chuo kinachotambuliwa na Serikali.

f) Kwa nafasi ya Mweka Hazina wa Chama, Mgombea ni lazima awe na shahada ya kwanza katika taaluma ya uhasibu kutoka chuo kinachotambuliwa na Serikali.

g) Wagombea wa nafasi ya Vijana; wahakikishe kwamba umri wao wakati wa kugombea uwawezeshe kukitumikia Chama si chini ya miaka mitano (5) baada ya kuchaguliwa kabla ya umri wa ujana wake kuisha.

**4.2 Nafasi za uongozi zinazogombewa katika ngazi ya Taifa:**

a) Mwenyekiti wa Chama wa Taifa.
b) Makamu Mwenyekiti wa Chama.
(k) Katibu Mkuu wa Chama.
(l) Naibu Katibu Mkuu wa Chama.
(m) Mweka Hazina wa Chama.
(n) Mwenyekiti na Katibu wa Kamati ya Ushauri ya Wafanyakazi Wanawake Taifa.
(o) Wajumbe kumi (10) wa Kamati ya Ushauri Wafanyakazi Wanawake Taifa kwa mchanganuo ufuatao:
    - Mjumbe mmoja mwakilishi wa Wafanyakazi wanawake wa Halmashauri za Majiji.
    - Mjumbe mmoja mwakilishi wa Mashirika ya Uchumi ya Halmashuri.
    - Mjumbe mmoja mwakilishi wa Wafanyakazi wanawake toka Halmashauri za Miji

- Mjumbe mmoja mwakilishi wa Wafanyakazi wanawake toka Halmashauri za Manispaa
- Wajumbe watatu (3) wawakilshi wa Wafanyakazi wanawake toka Halmashauri za Wilaya
- Wajumbe watatu (3) wanaowakilisha Wafanyakazi Wanawake kutoka miongoni mwa Wanachama wanaofanya kazi Serikali Kuu, Wakala na Taasisi za Serikali

(p) Wajumbe 16 wa kuingia kwenye Baraza Kuu la Shirikisho kwa kuzingatia Jinsia.

(q) Mjumbe mmoja kuingia kwenye Kamati ya Utendaji ya Shirikisho

(r) Wadhamini wanne (4) wa Chama.

(s) Mjumbe mmoja mwakilishi wa Wafanyakazi wenye ulemavu atakayechaguliwa miongoni mwa wawakilishi wa Mikoa kuingia kwenye Kamati ya Utendaji ya Taifa.

(t) Mjumbe mmoja mwakilishi wa Wafanyakazi vijana atakayechaguliwa miongoni mwa wawakilishi wa Mikoa kuingia kwenye Kamati ya Utendaji Taifa.

(u) Wajumbe wawili (2) watakaoingia kwenye Kamati ya Utendaji ya Taifa kutoka miongoni mwa Wanachama wanaofanya kazi Serikali Kuu, Wakala na Taasisi za Serikali.

(v) Wajumbe watatu (3) watakaoingia kwenye Baraza Kuu kutoka miongoni mwa Wanachama wanaofanya kazi Serikali Kuu, Wakala na Taasisi za Serikali.

(w) Wajumbe tisa (9) watakaoingia kwenye Mkutano Mkuu Taifa kutoka miongoni mwa Wanachama wanaofanya kazi Serikali Kuu, Wakala na Taasisi za Serikali.


➢ **MAMBO YA KUZINGATIA:**

Mwanachama anayetaka kugombea atatakiwa kuambatanisha nakala za vitu vifuatavyo:

1. Nakala ya hati ya malipo ya mshahara wa mwezi mmoja wa karibuni kabla ya uchaguzi.
2. Nakala ya cheti cha chuo kikuu kwa watakaogombea nafasi ya Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na Mweka Hazina wa Chama.
3. Cheti cha kuzaliwa kwa watakaogombea nafasi ya Vijana ( kwa mujibu wa Katiba ya Chama toleo la 2024 tafsiri ya kijana ni umri wa miaka 18 - 35).
4. Ili kuweza kugombea uongozi nafasi ya Mwenyekiti wa Wilaya, Mwakilishi wa Vijana Wilaya na Mwakilishi wa Wenyeulemavu Wilaya mgombea anapaswa kugombea uwakilishi wa nafasi kama hiyo kwenye ngazi ya Tawi.
5. Ili kuweza kugombea uongozi nafasi ya Mwakilishi wa Vijana Taifa na Mwakilishi wa Wenyeulemavu Taifa, mgombea anapaswa kugombea uwakilishi wa nafasi kama hiyo kwenye ngazi ya Mkoa.
6. Ili kuweza kugombea uongozi nafasi ya Mwakilishi wa Vijana Mkoa na Mwakilishi wa Wenyeulemavu Mkoa, mgombea anapaswa kugombea uwakilishi wa nafasi kama hiyo kwenye ngazi ya Wilaya.
7. Ili kuweza kugombea uongozi nafasi ya Mwakilishi wa Vijana Wilaya na Mwakilishi wa Wenyeulemavu Wilaya, mgombea anapaswa kugombea uwakilishi wa nafasi kama hiyo kwenye ngazi ya Tawi.
8. Ili kuweza kugombea nafasi ya mjumbe mmoja kutoka miongoni mwa Makatibu wa matawi atakayeingia kwenye Kamati ya Utendaji ya Wilaya, mgombea anapaswa kugombea nafasi ya Katibu wa Tawi.

**NB: Tangazo hili linapatikana pia katika tovuti yetu: www.talgwu.or.tz**

**Mshikamano, Daima**



……………………………

***Wandiba P. Ngocho***

**KAIMU KATIBU MKUU-TALGWU**